the pittsburgh promise

# HATI INAYOARIFU




## JE, NITAHITAJI NINI ILI NISTAHIKI?

**Ili wanafunzi wastahiki kwa mpango wa ufadhili wa masomo wa Pittsburgh Promise, lazima:**

1. wahitimu kutoka shule ya upili mnamo, au kabla ya, mwaka wa 2028
2. wawe wameandikishwa mfululizo, tangu angalau darasa la 9, katika Shule za Umma za Pittsburgh, au shule inayofadhiliwa na Shule za Umma za Pittsburgh
3. wawe wakazi wa Jiji la Pittsburgh (au Wilkinsburg), mfululizo, tangu angalau darasa la 9.
4. wahitimu kutoka shule ya upili ya PPS wakiwa na wastani wa alama zisizozingatia ugumu wa somo wa kiwango cha chini zaidi cha 2.50 na rekodi ya mahudhurio ya 90% au zaidi

Wanafunzi watakaokidhi mahitaji mengine ya mpango wa Promise, lakini watahitimu wakiwa na wastani wa alama zisizozingatia ugumu wa somo wa kiwango cha kati ya 2.0 na 2.49 wanaweza kuomba Mpango wa Mwendelezo wa Promise. Fedha za mpango wa Promise husaidia kulipia mpango, na watakaokamilisha mtaala wa mwaka mzima watastahiki kikamilifu kwa mpango wa Promise. Pata taarifa zaidi katika **pittsburghpromise.org/the-scholarship/eligibility**.

## NITAPATA PESA NGAPI ZA UFADHILI WA MASOMO YA CHUO?

**Wanafunzi wanaostahiki ambao wameandikisha mfululizo tangu siku ya kwanza yadarasa la 9 watastahiki kwa *hadi* $5,000 kwa mwaka (kiwango cha juu zaidi cha $20,000) inayopaswa kutumiwa ndani ya miaka mitano baada ya kuhitimu kutoka shule ya upili. *Kiwango cha chini zaidi cha ufadhili wa masomo* cha $1,000 kila mwaka kitatolewa kwa wanafunzi wote wanaostahiki na walioandikishwa**

Mpango wa ufadhili wa masomo wa Promise ni mpango unaohitaji utumie "pesa zote ulizopewa". Hii inamaanisha kuwa *hadi* $5,000 kwa mwaka (kiwango cha juu zaidi cha $20,000) itajumlishwa kwa Salio la mwanafunzi baada ya kutoa ruzuku za serikali (kama vile Pell, PHEAA, na FSEOG), ruzuku nyingine, na ufadhili wa masomo, ikiwa ni pamoja na ada unayolipiwa na chuo, kwa kila moja ya miaka mitano ya elimu ya baada ya sekondari.

Ikiwa mwanafunzi aliye na tuzo ya kiwango cha juu zaidi cha $ 5,000 anahitaji tu $ 3,000 ili alipie gharama zote, tunatoa $3,000. Ikiwa mwanafunzi hana gharama zozote baada ya kujumuisha ruzuku na ufadhili mwingine wowote, bado atapata tuzo ya kiwango cha chini zaidi cha $ 1,000 kutoka kwa Mpango wa Promise ili aitumie kulipia gharama zinazohusiana na shule kwa hiari yake.

## JE, UNAWEZA KUTUMIA **FEDHA ZA PROMISE** KUFANYA NINI?

**Kwa Wanafunzi wa 2018 kuendelea:**

Mpango wa fadhili wa masomo wa Promise husaidia kulipa Jumla ya Gharama ya Mahudhurio. Hii ni pamoja na masomo, ada, chumba, malazi, na vitabu.

## NINAWEZA KUTUMIA FEDHA ZA UFADHILI WA MASOMO WA MPANGO WA PROMISE WAPI?

Wanafunzi wanaweza kuhudhuria chuo chochote, chuo kikuu, shule ya biashara, au shule yoyote ya ufundi iliyoidhinishwa huko Pennsylvania, ikiwa ni pamoja na mipango ya mafundisho ya mtandaoni inayotolewa na shule hizi. Lazima mipango hiyo istahiki kwa ruzuku ya shirikisho ya Pell. Fedha za mpango wa Promise ni za elimu ya baada ya sekondari pekee, na hazipaswi kutumika kwa ajili ya mipango ya baada ya shahada ya kwanza. Mpango wa Promise haufadhili shule zinazotoa mafundisho mtandaoni pekee (zisizo na taasisi ya kudumu iliyoko Pennsylvania pekee).

## JE, NINAPASWA KUTUMIA FEDHA ZA UFADHILI WA MASOMO KWA MUDA GANI?

Fedha za Mpango wa Pittsburgh Promise lazima zitumike ndani ya miaka mitano baada ya kuhitimu kutoka shule ya upili.

## ITAKUWAJE IKIWA SITUZWI ALAMA KWA KUTUMIA KIPIMO CHA KAWAIDA CHA 4.0?

Shule za Umma za Pittsburgh zina jukumu la kutoa taarifa ya masomo ya kila mwanafunzi kwa Mpango wa Promise. Mshauri nasaha wako wa Mwongozo au Mpito atashirikiana na shule yako ili kubaini maendeleo yako ya masomo na kwa madhumuni ya kuona ikiwa unastahiki kwa mpango wa Promise.

## JE, IWAPO KUNA TATIZO LINALOATHIRI UANDIKISHAJI, GPA, MAHUDHURIO YANGU AU SUALA LINGINE LINALOATHIRI USTAHIKI WANGU KUTOKANA NA HALI AMBAZO SIWEZI KUDHIBITI?

Kuna mchakato wa Kukataa Rufaa ya Huruma kwa ajili ya wanafunzi walio na tatizo kubwa au suala linalowazuia kustahiki kupata ufadhili wa masomo. Rufaa huwasilishwa kupitia Kituo cha Wanafunzi cha mpango wa Promise. Rufaa huzingatiwa kwa misingi ya IEP, 504, na hali zingine ambazo mwanafunzi hawezi kudhibiti. Rufaa zinaweza kuwasilishwa mwanafunzi akiwa katika shule ya upili na chuo kikuu.

## NITAENDELEAJE KUSTAHIKI KWA MPANGO WA PROMISE BAADA YA KUANZA KUHUDHURIA SHULE YA BAADA YA SEKONDARI?

Wanafunzi lazima wadumishe wastani wa alama zote wa 2.0 na wakamilishe kozi ya muda wote kama inavyofafanuliwa na shule wanayohudhuria, kwa kawaida huwa wanahitaji alama 12-16. Wasiliana na shule yako ili ujue ufafanuzi wao wa muda wote. Maendeleo ya masomo yatakaguliwa na mpango wa Promise mwishoni mwa kila mwaka wa masomo. Mpango wa Promise haufadhili wanafunzi wanaojiandikisha kwa muda. *Kumbuka: Katika vyuo vingi vya miaka 4, wanafunzi lazima wamalize kozi 15 kwa kila muhula ili waweze kuhitimu baada ya miaka 4.*

Wanafunzi lazima wajaze maombi ya FAFSA (Maombi ya Bure ya Misaada ya Wanafunzi ya Shirikisho) kila mwaka wanapohudhuria shule ya baada ya sekondari kabla ya mpango wa Promise kushughulikiwa.

## JE, NINATUMA MAOMBI VIPI?

Katika kidato cha nne cha shule ya upili, ingia katika Kituo cha Wanafunzi cha Promise ili ujaze Hati ya FERPA na uingize shule unayokuvutia nayo(nazo).

## SHULE YANGU INAPATAJE MPANGO WA UFADHILI WA MASOMO WA PROMISE?

Wanafunzi huingiza jina la shule watakayohudhuria katika Kituo cha Wanafunzi cha Promise kisha mpango wa Promise hushughulikia mambo yanayohitajika. Shule hutumia Mpango wa Pittsburgh Promise bili ili wapate fedha. Cheki hutumwa moja kwa moja shuleni.

## JE, UNA MASWALI ZAIDI? WASILIANA NASI.

**412-281-7605** (simu)
**412-281-7638** (faksi)
**info@pittsburghpromise.org** (barua pepe)
**1901 Centre Avenue, Suite 204, Pittsburgh, PA 15219** (barua ya posta)

## ORODHA YA SHULE ZA UPILI ZINAZOSTAHIKI KWA MPANGO WA PROMISE

**City High Charter High School**
**Environmental Charter School**
**Passport Academy Charter School**
**Pittsburgh Allderdice**
**Pittsburgh Brashear**
**Pittsburgh CAPA**
**Pittsburgh Carrick**
**Pittsburgh Milliones (UPrep)**
**Pittsburgh Obama**
**Pittsburgh Online Academy***
**Pittsburgh Perry**
**Pittsburgh Sci-Tech Academy**
**Pittsburgh Westinghouse**
**The Academy Charter High School**
**Urban Pathways Charter High School**

*** *Pittsburgh Online Academy ndio shule pekee ya upili ya mafundisho ya mtandaoni ambao wanafunzi wake hustahiki kwa mpango wa ufadhili wa masomo wa Promise.*

the pittsburgh promise

Jifunze zaidi kuhusu mpango wa Pittsburgh Promise:
**www.pittsburghpromise.org**